



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيُسْتَخْلَفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَإِنْ يَعْلَمُنَّ هُمْ دِيَمَنَ الَّذِي أَرْضَى لَهُمْ وَلَيَسْبِدَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَوْهُمْ أَمَّا
يَعْبُدُونَ فَلَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Alhamisi, 13 Shawwal 1441 H

04/06/2020 M

Na: 1441/39

Taarifa kwa Vyombo vy ya Habari

Kufuatia Kuchapishwa kwa Taarifa kwa Vyombo vy ya Habari: "Kupeleka Majeshi ya Amerika Nchini Tunisia ni Shari Iliyo Enea" Idara ya Facebook Imeufunga Ukurasa wa Facebook wa Hizb ut Tahrir / Wilayah Tunisia (Imetafsiriwa)

Idara ya Facebook mnamo asubuhi ya 4 Juni iliufunga ukurasa wa Facebook wa Hizb ut Tahrir / Wilayah Tunisia, na ingawa ufungaji huu sio wa kwanza, na wala hautakuwa wa mwisho, ni muhimu kutaja kwamba ufungaji huu ulifanywa kufuatia taarifa kwa vyombo vy ya habari kwa anwani "Kupeleka Majeshi ya Amerika Nchini Tunisia ni Shari Iliyo Enea" ambayo kwayo Hizb ilionya dhidi ya kuingia kwa jeshi la Msalaba la Kiamerika nchini Tunisia, ambapo imefichua upande ambao idara ya Facebook inatangaza vita vyake viovu dhidi ya kurasa za Hizb ut Tahrir katika Facebook.

Taarifa ya hivi juzi kwa vyombo vy ya habari ya Hizb ut Tahrir / Wilayah Tunisia ilifichua dori ya uongozi wa Kijeshi wa Amerika barani Afrika (AFRICOM) ambao uliundwa ili kuitawala Afrika, kuifuja utajiri wake na kuwakoloni watu wake, zaidi ya hayo kupambana na Uislamu chini ya kisingizio cha kupambana na "ugaidi" kwa sababu unauna Uislamu kama tishio halisi la maslahi yake ya kiuchumi ulimwenguni, ikiwemo Afrika, ambayo wengi wa watu wake ni Waislamu. Vilevile, taarifa hiyo iliwaonya watu wa Tunisia dhidi ya kuruhusu kuingia kwa jeshi la Kiamerika nchini Tunisia, kwani pindi majeshi hayo ya Kiamerika yanapoingia katika nchini, huangamiza na kuufanya utukufu wa watu kuwa wake udhalilifu, na hivyo ndivyo wafanyakavyo. Taarifa hiyo ilitamatisha kuwa hakuna kitakachouzuia ulafi wa kikoloni wa Amerika na nchi zilizo salia za kikoloni za kikafiri za Kimaghribi na ufujaji wao wa mali ulimwengu mzima ikiwemo Afrika isipokuwa Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume, na pasi kwayo wanadamu wote wataendelea kuteseka kutohana na ulafi wa kikoloni na dhulma ya Urasilimali.

Idara ya Facebook kwa mara nyengine tena imethibitisha kwamba inazipendelea dola za kikoloni na ala zake za kieneo, na imethibitisha pasi na shaka yoyote kwamba hadhara ya Kimaghribi imeshindwa kukabiliana na Uislamu kifikra na kisiasa, hivyo daima hutumia mbinu za kuzuia na kufunga kama vile serikali za kiimla na huduma zake za kijasusi na licha ya kuzuia huku, Hizb ut Tahrir inaendelea kufikia lengo lake, haitazuiwa na dhulma za wenye kudhulamu wala mbinu za walio cheshewa.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[بِنْ تَقْدِفُ بِالْحُقْقِ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَنْمَعُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ وَلَكُمُ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ]

"Bali tunaitupa kweli juu ya uwongo ikauvunja na mara ukatoweka. Na ole wenu kwa mnayo yazua." [Al-Anbiya: 18].

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Tunisia